TBARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2015

# 07 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# KITABU CHA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI UPIMAJI WA KITAIFA DARASA LA NNE (SFNA) 2015

# 07 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Kimechapwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI....................................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ................................ 2

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua .................................................. 2

2.2 Sehemu B: Swali la Kuoanisha .................................................... 11

2.3 Sehemu C: Kuandika KWELI au SI KWELI ................................. 16

2.4 Sehemu D: Maswali ya Majibu Mafupi ....................................... 21

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KATIKA KILA MADA ILIYOPIMWA.. 26

4.0 HITIMISHO ............................................................................ 28

5.0 MAPENDEKEZO ..................................................................... 28

Kiambatisho A ............................................................................ 30

Kiambatisho B ............................................................................ 31

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Upimaji wa Darasa la Nne katika somo la TEHAMA imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali wakati wa upimaji wa kitaifa. Majibu ya wanafunzi katika upimaji huo ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha kiwango cha maarifa, stadi na mielekeo ambayo wanafunzi waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi.

Katika kitabu hiki, uchambuzi umeonesha mambo yaliyosababisha wanafunzi kutojibu maswali kwa ufanisi kama vile kushindwa kuelewa matakwa ya maswali; kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali, kushindwa kuhawilisha maarifa na kutofuata maelekezo ya upimaji. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliofanya vizuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali, kwa hiyo waliweza kuelewa matakwa ya maswali. Uchambuzi wa kila swali umefanyika na kasoro za wanafunzi katika kujibu maswali zimeoneshwa. Aidha, mada zenye ufaulu mzuri, wa wastani na hafifu katika upimaji wa kitaifa zimeoneshwa.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, mrejesho huu utawezesha wadau mbalimbali wa elimu kwa ujumla, na hasa mamlaka husika, kuchukua hatua stahiki katika kushughulikia kasoro zilizooneshwa katika kitabu hiki kwa nia ya kuboresha ufaulu katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) wa siku zijazo.

Mwisho, Baraza lingependa kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wote walioshiriki katika utayarishaji wa kitabu hiki. Baraza litathamini michango na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu, yanayolenga katika kuboresha vitabu vya siku zijazo.



**Dkt. Charles E. Msonde**
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2015 ulifanyika rasmi nchini tarehe 25 na 26 Novemba 2015. Jumla ya wanafunzi 174,859 walisajiliwa katika upimaji huo kwa somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kati ya wanafunzi waliosajiliwa, wanafunzi 173,317, sawa na asilimia 99.1, walifaulu katika upimaji huo.

Muundo wa karatasi ya maswali ya upimaji wa somo la TEHAMA ulikuwa umegawanyika katika sehemu nne; A, B, C na D zenye jumla ya maswali 25. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya kuchagua, ambapo wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya chaguzi nne walizokuwa wamepewa na kisha kuandika herufi ya jibu walilochagua katika kisanduku walichokuwa wamepewa katika swali hilo. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 20. Sehemu B ilikuwa na maswali matano (5) ya kuoanisha yenye jumla ya alama 10. Wanafunzi walitakiwa kuoanisha maelezo ya matumizi ya sehemu ya kompyuta kutoka fungu A na majina ya sehemu zinazounda kompyuta kutoka kifungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano yaliyo mbele ya kila swali. Sehemu C, ilikuwa na maswali matano ya “Kweli” au “Si Kweli” yaliyokuwa na jumla ya alama 5. Wanafunzi walitakiwa kujaza neno “KWELI” kama sentensi ilikuwa sahihi na neno “SI KWELI” kama sentensi haikuwa sahihi. Sehemu D ilikuwa na maswali matano (5) ya majibu mafupi. Wanafunzi walitakiwa kusoma swali na kisha kujaza jibu kwenye nafasi liyokuwa imeachwa wazi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15; alama 3 kwa kila swali.

Uchambuzi huu umefanyika kwa kuangalia swali mojamoja, namna lilivyojibiwa na sababu ambazo zimechangia kwa majibu hayo.

Uchambuzi huu unaweza kuwasaidia walimu na wanafunzi kufanya marekebisho hasa katika mada ambazo wanafunzi wameonekana kutofanya vizuri. Ufaulu wa wanafunzi ulikuwa 'Hafifu' kama wanafunzi walipata kati ya aisilimia 0 hadi 20 ya alama, 'Wastani' kama wanafunzi walipata kati ya asilimia 22 hadi 61 na 'Mzuri' kama wanafunzi walipata kati ya asilimia 62 hadi 100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua

Katika sehemu hii wanafunzi walitakiwa kusoma swali na kisha kuchagua jibu lililo sahihi kati ya chaguzi nne walizokuwa wamepewa. Aidha walitakiwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku walichokuwa wamepewa katika kila swali. Uchambuzi uliofanyika unabainisha idadi na asilimia ya wanafunzi waliochagua jibu sahihi, wanafunzi ambao hawakuweza kubaini jibu sahihi na sababu ambazo zinaweza kuwa zimesababisha uchaguzi huo.

**Swali la 1:** Simu ambazo hutumiwa na polisi ili kupeana taarifa zinaitwa

A simu za upepo
B simu za mkononi
C simu za mezani
D simu za intaneti

☐

Swali hili lilipima maarifa ya wanafunzi kuhusu matumizi ya namba maalum za simu zinazotumika katika mawasiliano ya dharura kama vile moto. Mwanafunzi alitarajiwa kufahamu kuwa simu ya upepo ni mahususi kwa matumizi ya polisi katika kazi zao za kila siku. Swali hili lilijibiwa kwa kiwango kisichoridhisha kwani wanafunzi 62,735, sawa na asilimia 35.9 tu, waliweza kuchagua "A: Simu za Upepo"

ambalo lilikuwa jibu sahihi. Jibu hilo kuchaguliwa kwa kiwango kisichoridhisha inaashiria ufinyu wa maarifa wa wanafunzi kuhusu matumizi ya simu katika mawasiliano, hasa simu zinazotumiwa na makundi maalumu kama vile jeshi la polisi. Aidha, wanafunzi 112,054, sawa na asilimia 64.1, walichagua kati ya vipotoshi B, C na D ambacho ni kielelezo kwamba hawana stadi za uchambuzi, hasa unaohusu aina mbalimbali za simu na matumizi yake. Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi umeoneshwa kwa ufupi katika jedwali Na 1.

**Jedwali Na 1:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 1

| Jumla ya wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 62,739 | 35.9 | 112,089 | 64.08 | 35 | 0.02 |

**Swali la 2:** Namba ya simu ambayo hutumiwa na watu kwenye matukio ya hatari kama moto ni

A 113
B 112
C 110
D 114

Swali hili lilikuwa linapima uwezo wa wanafunzi kutambua namba maalumu zinazotumika katika masuala ya dharura hususan matukio ya moto. Wanafunzi walikuwa wamepewa namba mbalimbali zinazoweza kupigwa wakati wa dharura, ili waweze kutambua namba ya simu inayotumika katika matukio ya hatari kama vile moto. Swali hili lilijibiwa kwa kiwango cha wastani. Jumla ya wanafunzi 76,454, sawa na asilimia 43.7, waliweza kuchagua “B: 112” ambalo ni jibu sahihi. Hata hivyo, wanafunzi 98,390, sawa na asilimia 56.2, hawakuweza kubaini jibu sahihi. Uchambuzi zaidi

umeonesha kuwa, wapo wanafunzi walioonekana kutokuwa na uhakika kwa kuchagua kipotoshi A, C na D, jambo linalooonesha ukosefu wa maarifa ya namba mbalimbali za kupiga wakati wa dharura. Jedwali Na. 2.1.2 linaonesha mchanganuo wa majibu ya watahiniwa.

**Jedwali Na 2:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 2

| Jumla ya Wanafunzi | waliopata | % | waliokosa | % | wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 76,454 | 43.7 | 98,390 | 56.2 | 15 | 0.1 |

**Swali la 3:** Kifaa kipi kati ya vifuatavyo hutumika kutengenezea ngoma?

A Plastiki
B Kitambaa
C Ngozi
D Mwanzi

Swali hili lilipima ufahamu wa wanafunzi kuhusu kifaa kinachotumika katika utengenezaji wa ngoma. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri sana. Hii iliashiria kwamba wanafunzi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utengenezaji wa ngoma. Kama jedwali Na 3 linavyoonesha, asilimia 89.7 ya wanafunzi walichagua jibu sahihi. Ni asilimia 10.2 tu ya wanafunzi ndio walichagua majibu A, B na D ambayo hayakuwa sahihi. Majibu haya ni ushahidi kuwa wanafunzi hao wachache hawakuwa na uelewa wala maarifa ya kutosha kuhusu vifaa vinavyotumika kutengeneza ngoma. Kutokana na ukosefu huo wa maarifa wanafunzi walijibu kwa kubahatisha na kuchagua majibu yasiyo sahihi. Jedwali Na. 3 linaonesha uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kitakwimu.

**Jedwali Na 3:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 3

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 159,930 | 89.7 | 17,920 | 10.2 | 9 | 0.1 |

**Swali la 4:** Kipande cha karatasi chenye maandiko yenye ujumbe maalumu ambacho hutumika kwa matangazo ya muda mfupi kinaitwa

A bango

B kipeperushi

C gazeti

D makala

Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kubaini jina la kipande cha karatasi chenye maandishi yenye ujumbe maalumu ambacho hutumika kwa matangazo ya muda mfupi. Ili kujibu swali hili kwa ufasaha, wanafunzi walitakiwa kujua njia mbalimbali zinazotumika kuwasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 90,081, sawa na asilimia 51.5, walichagua "B: kipeperushi", ambalo ni jibu sahihi. Majibu ya wanafunzi hao yaliashiria kuwa walikuwa na maarifa na uelewa wa kutosha kuhusu mawasiliano kwa njia ya maandiko. Hata hivyo ni wazi kuwa karibu nusu ya wanafunzi walioshiriki katika upimaji walikuwa na uelewa finyu kuhusu njia za mawasiliano ya maandishi zitumikazo kutoa ujumbe kwa muda mfupi. Kutokuwa na uelewa wa kutosha kulifanya wanafunzi 84,769, sawa na asilimia 48.5, kushindwa kubaini jibu sahihi na hivyo kuchagua vipotoshi A, C na D. Kielelezo Na 2.1.1 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya wanafunzi ambapo zaidi kidogo ya nusu (51.5%) ya wanafunzi waliweza kubaini jibu sahihi na waliobaki hawakuweza kuchagua jibu sahihi.




***Kielelezo Na 1***: Ufaulu wa wastani katika swali ambapo asilimia 51.5 waliweza kuchagua jibu sahihi.

**Swali la 5:** Kituo kipi kati ya vifuatavyo hutumika kutoa ushauri nasaha hapa Tanzania?

A ANGAZA

B SHIDEPHA

C WAMA

D EMAU

Katika swali hili lililotokana na mada ya "Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano", wanafunzi walitakiwa kuchagua jina mojawapo la kituo kinachotumika kutoa ushauri nasaha hapa nchini kutoka katika orodha ya vituo vinne walivyokuwa wamepewa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 104,595, sawa na asilimia 59.8, waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni "A: ANGAZA". Wanafunzi hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vituo vya ushauri nasaha ambayo yaliwawezesha kukitofautisha na mashirika na taasisi nyingine. Aidha, wanafunzi 70,258, sawa na asilimia 40.2 walishindwa kubaini jibu sahihi. Hiki ni

kiashiria cha kutokuwa na maarifa ya kutosha yaliyowafanya washindwe kupambanua kituo cha ushauri nasaha na taasisi nyingine. Jedwali Na 4 linaonesha takwimu za wanafunzi na majibu yao na asilimia za wanafunzi walioweza kujibu swali hili.

**Jedwali Na 4:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 5

| Jumla ya wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 104,495 | 59.8 | 70,258 | 40.2 | 6 | 0.0 |

**Swali la 6:** Nyumba au chumba kinachotunza vitabu na maandiko mengine kinaitwa

A maktaba
B nyumba ya vitabu
C chumba cha vitabu
D stoo ya vitabu

Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya chaguzi A, B, C na D. Majibu ya swali hili yalitegemea ujuzi wa mwanafunzi katika matumizi ya maktaba ambayo yangemwezesha kujua kuwa vitabu na maandiko mbalimbali yanapatikana maktaba. Jumla ya wanafunzi 174,859 walijibu swali hilo ambapo, wanafunzi 158,372 (90.6%), waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni "A: maktaba". Aidha, wanafunzi 16,476 (9.4%) walichagua vipotoshi B, C na D, jambo linalonesha hawakuwa na maarifa kuhusu maktaba na matumizi yake. Wanafunzi 11 tu ndio ambao hawakufanya swali hilo.

**Jedwali Na 5:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 6

| Jumla ya wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 158,372 | 90.6 | 16,476 | 9.4 | 0 | 0.0 |

**Swali la 7:** Kipi kati ya vifuatavyo siyo chombo cha mawasiliano?

A Kamera

B Radio

C Luninga

D Magazeti

Katika swali hili la 7, wanafunzi walitakiwa kubainisha chombo ambacho si cha mawasiliano kati ya vyombo walivyokuwa wamepewa kwenye chaguzi. Swali hili lilitokana na mada ya matumizi ya vyombo vya habari. Wanafunzi katika swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri, ambapo wanafunzi 121,993, sawa na asilimia 69.8, waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni "A: Kamera". Uchaguzi wa jibu sahihi ulionesha kuwa wanafunzi hao wana ufahamu wa kutosha uliowawezesha kutofautisha kati ya vyombo vinavyotumika kukusanya taarifa kabla hazijatawanywa na vyombo vinavyotumika kusambaza taarifa, yaani vyombo vya mawasiliano. Hata hivyo, wanafunzi 52,857 sawa na asilimia 30.2, walishindwa kubaini jibu sahihi na hivyo kuchagua vipotoshi B, C na D. Uchaguzi wa vipotoshi ni kielelezo cha ukosefu wa maarifa katika mada hiyo. Kushindwa kuchagua jibu sahihi pia kunaweza kuwa kulichangiwa na wanafunzi hao kutoelewa matakwa ya swali hilo. Jedwali Na. 6 linaonesha majibu ya wanafunzi na ufaulu wao katika asilimia.

**Jedwali Na.6:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 7

| Jumla ya wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 121,993 | 69.8 | 52,887 | 30.2 | 4 | 0.0 |

**Swali la 8:** Shirika la simu la Tanzania linalotoa huduma ya simu za mezani linaitwa

A Vodacom

B Tigo

C TTCL

D Nokia

Wanafunzi katika swali hili walitakiwa kuchagua jina la kampuni ya simu inayotoa huduma ya simu za mezani hapa Tanzania. Ili wanafunzi waweze kuchagua jibu sahihi walitakiwa kuwa na ufahamu wa makampuni yanayotoa huduma ya mawasiliano kwa njia ya simu na aina ya simu zinazotumika. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri. Jumla ya wanafunzi 111,543, sawa na asilimia 63.6, walichagua jibu sahihi ambalo ni "C: TTCL". Uchaguzi huu ulionesha kuwa wanafunzi wana maarifa ya kutosha ya kampuni za simu zinazotoa huduma hapa nchini pamoja na aina za simu zinazotumika. Aidha, kufanya vizuri kwa wanafunzi katika swali hili kunaweza kuwa kumesababishwa pia na ukweli kwamba simu za mezani zipo pia katika shule nyingi, hivyo wanafunzi walio wengi wanazifahamu, licha ya kuzisoma vitabuni. Hata hivyo, wanafunzi 63,295, sawa na asilimia 36.2, walishindwa kuchagua jibu sahihi. Wanafunzi hao walichagua vipotoshi "A: Vodacom", na "B: Tigo" ambazo ni kampuni zinazotoa huduma ya simu za mikononi. Aidha, baadhi walichagua "D: Nokia" ambayo ni kampuni ya kutengeneza simu. Uchaguzi wa vipotoshi wa wanafunzi hao unadhihirisha uwezo mdogo wa wanafunzi hao wa kutofautisha huduma zinazotolewa na kampuni mbalimbali za simu, ambacho ni kielelezo cha ufinyu wa maarifa. Jedwali Na. 7 linaonesha takwimu za majibu ya wanafunzi na kiwango cha ufaulu wao.

**Jedwali Na 7:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 8.

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 111,643 | 63.6 | 63,299 | 36.2 | 17 | 0.0 |

**Swali la 9:** Mwitiko maana yake ni hali ya upokeaji wa ___________

A Ujumbe

B Maneno

C Maelezo

D Vitendo

Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuchagua neno linalowakilisha maana ya mwitiko. Swali hili lilihitaji mwanafunzi awe na uelewa wa kutosha kuhusu njia mbalimbali za mawasiliano na namna ambavyo hutumika kufikisha na kupokea ujumbe. Swali hili lilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi wengi, ambapo wanafunzi 127,258, sawa na asilimia 72.8, walichagua jibu sahihi ambalo ni "A: Ujumbe". Uchaguzi wa jibu hilo umeonesha kuwa wanafunzi walikuwa na uelewa mzuri wa njia za mawasiliano na namna watu wanavyoitikia kuonesha kuwa wamepokea ujumbe au taarifa husika. Pamoja na wanafunzi wengi kufanya vizuri katika swali hili, wanafunzi 47,589, sawa na asilimia 27.2, walishindwa kubaini jibu sahihi. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuelewa swali au hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, ambayo yangewawezesha kubaini jibu sahihi. Jedwali Na 8 linaonesha idadi na asilimia ya wanafunzi ambao walichagua jibu sahihi na wale walioshindwa kubaini jibu hilo.

**Jedwali Na 8** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 9

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 127,258 | 72.8 | 47,589 | 27.2 | 12 | 0.0 |

**Swali la 10:** Neno au namba za siri ambazo humwezesha mtu kufungua kompyuta huitwa

A kiteuzi

*B microsoft*

C faksi

*D password*

Katika swali la 10 mwanafunzi alitakiwa kuchagua jina la neno la siri linaloandikwa wakati wa kufungua kompyuta. Katika kujibu swali hili, mwanafunzi alitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua za kufungua kompyuta kwa ajili ya matumizi. Wanafunzi walifaulu swali hili kwa kiwango cha wastani kwani wanafunzi 78,753 sawa na asilimia 45.0, waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni “D Password”. Wanafunzi 96,090 (55%), walishindwa kubaini jibu sahihi. Wanafunzi wachache kuweza kujibu kwa usahihi inaonesha changamoto iliyopo katika matumizi ya kompyuta. Kwa kuwa nywira ni kitu ambacho ni cha lazima kwenye kompyuta nyingi za kisasa, kushindwa kwa wanafunzi kubaini jibu sahihi ni ishara ya kutokuwa na ujuzi wa matumizi ya kompyuta. Jedwali Na. 9 linaonesha majibu ya wanafunzi na asilimia zao za kupata na kukosa swali hilo.

**Jedwali Na 9:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 10.

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 78,753 | 45.0 | 96,099 | 55 | 7 | 0.0 |

## 2.2 Sehemu B: Swali la Kuoanisha

Katika swali la 11 hadi la 15 katika sehemu hii, mwanafunzi alitakiwa kuoanisha maelezo ya matumizi ya sehemu za kompyuta katika kifungu A na majina ya sehemu hizo katika kifungu B kama

yanavyoonekana kwenye jedwali, kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano waliyokuwa wamepewa.

| Na | Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|---|
| 11. | Hutumika kupokea na kuchambua kazi zote zinazoingia kwenye kompyuta | (   ) | A. Kiteuzi/mausi |
| 12. | Hutumika kuchapa maandishi ya kompyuta kwenye karatasi. | (   ) | B. Kibodi |
| 13. | Hutumika kuonyesha taarifa iliyomo ndani ya kompyuta. | (   ) | C. Spika |
| 14. | Hutumika kuingiza maelekezo kwenye kompyuta. | (   ) | D. Printa |
| 15. | Hutumika kutoa sauti kwenye kompyuta. | (   ) | E. Kichakato kikuu |
| | | | F. Skrini |
| | | | G. Ghala |
| | | | H. Diskimwako |

Katika swali la 11, wanafunzi walitakiwa kubaini kitu ambacho "hutumika kupokea na kuchambua kazi zote zinazoingia kwenye kompyuta". Katika kujibu swali hili, mwanafunzi alitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha wa mfumo wa kompyuta. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu sana kwani ni wanafunzi 127,302, sawa na asilimia 72.8, walioshindwa kuoanisha maelezo hayo na kifaa sahihi ambacho ni "E: Kichakato Kikuu". Kichakato Kikuu ndiyo sehemu muhimu kwenye kompyuta inayowezesha kufanya kazi zote zinazoingizwa kwenye kompyuta kwa ajili ya kuchakatwa. Kushindwa kwa wanafunzi wengi kubaini jibu sahihi ni kielelezo kuwa wanafunzi hawana ujuzi wa matumizi ya kompyuta hususan

mfumo na ufanyaji kazi wa kompyuta. Aidha, wanafunzi 47,549, sawa na asilimia 27.2, waliweza kuoanisha maelezo hayo na kifaa sahihi. Wanafunzi hao wachache walionesha kuwa na ujuzi wa kutosha wa mfumo wa kompyuta. Mchanganuo wa majibu ya wanafunzi umeoneshwa katika jedwali Na 10.

**Jedwali Na 10:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 11

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 47,549 | 27.2 | 127,302 | 72.8 | 8 | 0.1 |

Maelezo ya swali la 12 yalikuwa yanasomeka kama ifuatavyo: “Hutumika kuchapa maandishi ya kompyuta kwenye karatasi”. Swali hili lilipima pia ujuzi na stadi za mwanafunzi katika matumizi ya kompyuta. Mwanafunzi alitakiwa kujua ni namna gani maandishi au kazi iliyofanyika ndani ya kompyuta huweza kuchapwa kwenye karatasi. Ufaulu katika swali hili pia ulikuwa hafifu kwani wanafunzi 114, 867, sawa na asilimia 65.7, walishindwa kuoanisha maelezo hayo na kifaa husika ambacho ni “D: Printa”. Kushindwa kwa wanafunzi wengi kwa kiasi hicho kubaini kuwa printa ndiyo inayotumika kuchapa maandishi kwenye karatasi ni kielelezo kuwa ujuzi wa wanafunzi katika matumizi ya kompyuta ni hafifu. Hali hiyo pia inaashiria kuwa wanafunzi hawajui sehemu mbalimbali za kompyuta na uhusiano wake katika kufanya kazi. Aidha, ni wanafunzi 59,985, sawa na asilimia 34.3, walioweza kuoanisha maelezo hayo na kifaa husika kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na 11.

**Jedwali Na 11:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 12

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,867 | 59,985 | 34.3 | 114,853 | 65.7 | 7 | 0.1 |

Maelezo ya swali la 13 yalikuwa kama ifuatavyo: “hutumika kuonyesha taarifa iliyomo ndani ya kompyuta”. Katika swali hili, mwanafunzi alitakiwa kuoanisha maelezo haya na kifaa au sehemu ya kompyuta inayotumika kwa kazi hiyo. Kwa maana hiyo, ujuzi wa mwanafunzi katika matumizi ya kompyuta ulikuwa muhimu ili kumwezesha kujibu swali hili kwa ufasaha. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa hafifu pia. Wanafunzi 115,317, sawa na asilimia 65.9, walishindwa kuoanisha maelezo hayo na kifaa sahihi ambacho ni “F: Skrini”. Kushindwa huko ni kielelezo cha kutokuwa na ujuzi wa matumizi ya kompyuta kwa wanafunzi walio wengi. Skrini ni kifaa cha lazima katika kompyuta ambacho hutumika kumwezesha mtumiaji kuona taarifa zilizopo ndani ya kompyuta. Kwa hiyo basi wanafunzi wengi kukosa swali hili ni ushahidi kuwa hawana mazoea ya kutumia kifaa hicho. Kwa upande mwingine, wanafunzi 59,538, sawa na asilimia 34.0, waliweza kuoanisha maelezo hayo na kifaa sahihi. Hii ilionesha kuwa walikuwa na ufahamu na ujuzi wa sehemu mbalimbali za kompyuta. Jedwali Na. 12 linaonesha takwimu za ufaulu wa wanafunzi.

**Jedwali Na 12:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 13

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 59,538 | 34.0 | 115,317 | 65.9 | 7 | 0.0 |

Swali la 14 lilikuwa na maelezo yaliyosomeka kama ifuatavyo: “Hutumika kuingiza maelekezo kwenye kompyuta”. Wanafunzi katika

swali hili walitakiwa kuoanisha maelezo haya na kifaa kinachotumika kuingiza maelezo kwenye kompyuta au kazi nyingine zozote. Hili pia lilikuwa swali linalohitaji mwanafunzi awe na ujuzi wa matumizi ya kompyuta. Katika swali hili, wanafunzi 134,833, sawa na asiliimia 77.0, hawakuweza kuoanisha maelezo hayo na kifaa husika. Kushindwa kuoanisha huko kunaashiria kuwa wanafunzi hawana ujuzi wa matumizi ya kompyuta na hivyo kutoweza kujua ni sehemu gani hutumika kuingiza maelezo kwenye kompyuta. Kwa upande mwingine, wanafunzi 40,005, sawa na asilimia 22.9 tu, ndio walioweza kuoanisha maelezo hayo na jibu sahihi ambalo ni “B: Kibodi”. Kuweza kwao kuoanisha maelezo hayo na kifaa sahihi ni kielelezo cha maarifa waliyo nayo au ujuzi wao katika matumizi ya kompyuta. Jedwali Na. 13 linaonesha majibu ya wanafunzi katika swali hilo.

**Jedwali Na 13:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 14

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 40,005 | 22.9 | 134,7833 | 77.0 | 21 | 0.0 |

Swali la 15 lilikuwa swali la mwisho katika maswali ya kuoanisha. Maelezo ya swali hilo yalikuwa kama ifuatavyo: “Hutumika kutoa sauti kwenye kompyuta.” Hili pia lilikuwa swali lililohusu kuoanisha kazi ya kifaa au sehemu ya kompyuta na jina la kifaa husika. Swali hili lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu kifaa kinachotumika kutoa sauti kwenye kompyuta. Ili mwanafunzi aweze kujibu vizuri alitakiwa kuwa na ujuzi wa sehemu mbalimbali zinazounda mfumo wa komputa. Swali hili lilijibiwa kwa kiwango kizuri zaidi kuliko maswali yote katika sehemu hii. Jumla ya wanafunzi 120,968, sawa na asilimia 69.2, waliweza kuonanisha

maelezo hayo na kifaa sahihi ambacho ni “C: Spika”. Kwa kuwa spika hutumika pia katika vifaa vingine vya mawasiliano kama vile redio wanafunzi waliofanya vizuri waliweza kuhawilisha maarifa na hivyo kuweza kufahamu matumizi ya kifaa hicho kwenye kompyuta. Takwimu zinaonesha wanafunzi 53,878, sawa na asilimia 30.8, walishindwa kuoanisha maelezo hayo na kifaa au sehemu husika ya kompyuta, hali inayoashiria kutokuwa na ujuzi na maarifa katika matumizi ya kompyuta. Jedwali Na 14 linaonesha majibu ya wanafunzi.

**Jedwali Na 14:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 15

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 120,968 | 69.2 | 53,878 | 30.8 | 13 | 0.0 |

## 2.3 Sehemu C: Kuandika KWELI au SI KWELI

Katika sehemu **C** (swali la 16 - 20) wanafunzi walitakiwa kujibu maswali kwa kuandika **KWELI** au **SI KWELI** mwishoni mwa sentensi. Wanafunzi walitakiwa kuandika KWELI kama sentensi hiyo iliwasilisha maudhui sahihi, na SI KWELI kama sentensi hiyo iliwasilisha maudhui ambayo si sahihi. Mchanganuo wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali ni kama ifuatavyo:

**Swali la 16:** Mayowe hutumika katika sherehe. ____________

Swali hili lilipima ufahamu wa wanafunzi kuhusu matumizi ya mayowe kama njia ya mawasiliano. Swali hili lilijibiwa vizuri na wanafunzi kwani wanafunzi 131,538, sawa na asilimia 75.2, walijibu SI KWELI ambalo ni jibu sahihi. Hili ni jibu sahihi kwa kuwa mayowe kama njia ya mawasiliano hutumika wakati wa dharura. Watu

walioko kwenye hali ya hatari hupiga mayowe ili kuomba msaada kwa watu wengine. Kufanya vizuri kwa wanafunzi katika swali hili kumechangiwa na ukweli kwamba mayowe hutumika kwenye jamii. Kwa hiyo, pamoja na kujifunza shuleni, maarifa ya wanafunzi pia yameongezewa na ukweli huo. Ni wanafunzi 43,310 tu, sawa na asilimia 24.8, ndio waliojibu KWELI. Majibu ya wanafunzi hao yalionesha uwezo mdogo wa kutofautisha nderemo na vifijo vinavyoweza kusikika kwenye sherehe na mayowe ambayo kwa asili yake huashiria hatari. Majibu ya wanafunzi yameainishwa kwa ufupi kwenye jedwali Na 15.

**Jedwali Na 15:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 16

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 131,538 | 75.2 | 43,310 | 24.8 | 11 | 0.0 |

**Swali 17:** Alama za barabarani huonesha namna bora ya kutumia barabara. ______

Swali hili lilipima ufahamu wa wanafunzi wa matumizi ya alama kama njia ya mawasiliano. Wanafunzi walipaswa kujua kuwa alama za barabarani ni muhimu kwa watumiaji wa barabara kwani huwatahadharisha wakati wa kutumia barabara. Swali hili pia lilijibiwa vizuri sana na wanafunzi. Wanafunzi 149,819, sawa na asilimia 85.7, walijibu “KWELI” ambalo ni jibu sahihi. Ufaulu wa kiwango hiki umeonesha kuwa wanafunzi wana uelewa mzuri wa matumizi ya alama, hasa alama za barabarani. Hii imesababishwa na ukweli kuwa pamoja na alama hizo kufundishwa shuleni, wanafunzi hao ni sehemu ya jamii ambayo hutumia alama hizo. Kwa upande mwingine, wanafunzi 25,034, sawa na asilimia 14.3, walijibu “SI KWELI” ambalo halikuwa jibu sahihi. Wanafunzi hao kushindwa

kujibu kwa usahihi kunaashiria kutokuwa na uelewa kuhusu alama za barabarani. Jedwali Na. 16 linaonesha mchanganuo wa majibu ya wanafunzi.

**Jedwali Na 16:** Majibu ya Wanafunzi katika Swali la 17.

| Jumla ya Wanafunzi | Waliopata | % | Waliokosa | % | Wasiojibu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 174,859 | 149,819 | 85.7 | 25,034 | 14.3 | 6 | 0.0 |

**Swali 18:** Maandiko yanaweza kupangwa katika maktaba kulingana na mwandishi wa andiko. __________

Swali hili lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu kanuni za kupanga maandiko katika maktaba. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 112,858, sawa na asilimia 64.6, walijibu “KWELI”, ambalo ni jibu sahihi. Wanafunzi hao walionesha kuwa na ujuzi na maarifa ya matumizi ya maktaba, kitu kilichowasaidia katika kutambua ukweli wa sentensi hiyo. Kwa upande mwingine, wanafunzi 54,281, sawa na asilimia 31.0, walijibu “SI KWELI”, ambalo halikuwa jibu sahihi. Hii inaweza kuwa ilisababishwa na wanafunzi hao kutokuwa na uelewa wa kutosha na hivyo kushindwa kujibu kwa ufasaha. Wanafunzi wengine 7,620, sawa na asilimia 4.4, hawakujibu swali hilo. Majibu ya wanafunzi waliopata na kukosa swali hilo yameainishwa kwenye kielelezo Na. 2.




***Kielelezo Na. 2***: Ufaulu mzuri kwenye swali hili: asilimia 64.6 ya wanafunzi.

**Swali 19:** Filimbi ni njia ya kisasa ya mawasiliano __________

Swali lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu njia za mawasiliano. Wanafunzi walitarajiwa kuweza kutofautisha njia za kisasa za mawasiliano na njia za asili. Maarifa na ujuzi wa njia mbalimbali za mawasiliano za kisasa na za asili yalikuwa muhimu katika kuweza kujibu swali hili. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 93,887, sawa na asilimia 53.7, walijibu "SI KWELI", ambalo ni jibu sahihi. Jibu hilo lilionesha kuwa wanafunzi wengi wana maarifa ya kutosha yanayowawezesha kutofautisha kati ya njia za kisasa za mawasiliano na za asili. Kwa upande mwingine, wanafunzi 73,344, sawa na asilimia 41.9, walijibu "KWELI", ambalo halikuwa jibu sahihi kutokana na kutokuwa na maarifa yakutosha kuhusu njia za mawasiliano. Wanafunzi wengine 7,628, sawa na asilimia 4.4, hawakufanya swali hilo. Mchanganuo wa majibu ya wanafunzi umeoneshwa kwenye kielelezo Na. 3.




***Kielelezo Na. 3:*** Ufaulu wa wastani katika swali hili: aslimia 53.7 ya wanafunzi.

**Swali la 20:** Kompyuta nyingi hutumia programu andishi ya Microsoft word _____

Swali lililenga kupima ujuzi wa wanafunzi kuhusu maarifa na uelewa walionao wa programu mbalimbali zinazotumika katika uchapaji kwenye kompyuta. Kompyuta nyingi hapa nchini zinatumia programu andishi ya *Microsoft word* kama program muhimu kwenye kompyuta hizo. Ufaulu wa swali hilo ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 111,895, sawa na asilimia 64.0, walijibu kwa kuandika “KWELI”, ambalo ndio jibu sahihi. Wanafunzi hao walionesha kuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha wa matumizi ya programu andishi ya *Microsoft word.* Kwa upande mwingine, wanafunzi 55,342, sawa na asilimia 31.6, walijibu kwa kuandika “SI KWELI”, ambalo halikuwa jibu sahihi. Hali hiyo inaashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya programu za kompyuta na hivyo kutojua programu andishi inayotumiwa zaidi katika uchapaji. Takwimu zinaonesha wanafunzi 7,621, sawa na asilimia 4.4,

hawakujibu swali hili. Kilelelezo Na. 4 kinaonesha muhtasari wa majibu ya wanafunzi katika swali hilo.




***Kielelezo Na 4:*** Ufaulu mzuri wa wanafunzi unaofikia asilimia 64.0.

## 2.4 Sehemu D: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa ya majibu mafupi. Wanafunzi walitakiwa kusoma swali ambalo lilikuwa na sehemu iliyoachwa wazi na kisha kujaza jibu lake. Kwa ujumla, ufaulu katika sehemu hii ulikuwa hafifu. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ni kama ifuatatavyo:

**Swali la 21:** Kifaa kinachotumika kuingiza umeme kwenye betri ya simu ya mkononi kinaitwa ____________

Swali hili lilipima maarifa ya wanafunzi juu ya matumizi ya simu za mikononi na namna simu hizo zinavyopata nguvu ya umeme. Ili mwanafunzi aweze kujibu swali hili ilibidi awe na maarifa na ujuzi wa matumizi ya simu hizo, hususan namna simu hizo zinavyojazwa nguvu za umeme. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa hafifu sana kwani wanafunzi 38,830, sawa na asilimia 22.2, ndio

waliweza kujaza jibu sahihi ambalo ni “chaja”. Wanafunzi wengine 128,409, sawa na asilimia 73.4, hawakuweza kujaza jibu sahihi. Kilichosababisha wanafunzi hao kushindwa kutoa jibu sahihi ni pamoja na ukosefu wa maarifa kuhusu namna betri za simu zinavyowekewa umeme. Vilevile, kulikuwa na wanafunzi ambao walibainika kutojua kuandika kwani waliandika vitu ambavyo havikuweza kusomeka kwa urahisi. Wanafunzi wengine 7,620, sawa na asilimia 4.4, hawakujibu swali hilo. Mchanganuo wa majibu ya wanafunzi umeainishwa kwenye kielelezo Na 5.




***Kielelezo Na 5:*** *U*faulu hafifu wa asilimia 22.2 ya wanafunzi.

**Swali la 22:** Barua zimegawanyika katika mafungu mawili ambayo ni barua ya kirafiki na ___________

Swali lilipima ufahamu wa wanafunzi kuhusu aina ya mawasiliano kwa njia ya maandiko. Wanafunzi walitarajiwa kuwa na maarifa na ujuzi wa aina mbalimbali za mawasiliano kwa njia ya maandishi hususan mawasiliano kwa njia ya barua. Pamoja na swali hilo kuwa la moja kwa moja, ambapo mwanafunzi alihitaji kukumbuka tu aina

za barua, bado ufaulu wake haukuwa wa kuridhisha. Wanafunzi 64,122, sawa na asilimia 36.7, waliweza kuandika jibu sahihi ambalo ni barua ya kikazi. Aidha, wanafunzi 103,156, sawa na asilimia 59.0, hawakuweza kuandika jibu sahihi. Sababu za wanafunzi hao kushindwa kujibu kwa usahihi ni kutokuwa na uelewa katika mada hiyo. Pia wapo wanafunzi waliobainika kutokuwa na stadi za kutosha za kuandika. Wanafunzi wengine 7,621 sawa na asilimia 4.4, hawakujibu swali hili.  Mchanganuo wa majibu ya wanafunzi umeoneshwa kwenye kielelezo Na 6.




***Kielelezo Na 6***: Ufaulu usioridhisha wa asilimia 36.7.

**Swali la 23:** Hatua ya kwanza ya kutuma ujumbe kwa njia ya faksi ni ________

Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kubainisha hatua ya kwanza katika kutuma ujumbe kwa njia ya faksi. Jumla ya wanafunzi 167,160 walijibu swali hilo ambapo wanafunzi 164,407, sawa na asilimia 94.0, walishindwa kutoa jibu sahihi ambalo ni “kutayarisha ujumbe uanotaka kutuma”. Baadhi yao waliandika maneno kama

kutuma barua, kupiga simu na wenigne waliandika kutuma ujumbe kwa kutumia simu.  Wanafunzi hao wanaonekana kutokuwa na uelewa juu ya hatua za kufuata wakati wa kutuma ujumbe kwa njia ya faksi. Wanafunzi wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu ambayo yalikuwa kinyume na swali lillivyouliza. Aidha, wanafunzi 2,831 pekee, sawa na asilimia 1.6, ndio walioweza kujibu swali hili kwa usahihi. Hii ni ishara kuwa wanafunzi wachache tu ndio wenye uelewa wa matumizi ya faksi. Aidha, wanafunzi 7,699, sawa na asilimia 4.4, hawakujibu swali hilo.




**Kielelezo Na 7**: Ufaulu hafifu wa asilimia 1.6 tu ya wanafunzi.

**Swali la 24:** Mchoro huu ufuatao huitwa ___________



Mchoro unaotajwa katika swali ulikuwa wa simu ya mezani. Swali hili lilihitaji wanafunzi kuwa na uwezo wa kutambua maumbo ya aina mbalimbali za simu na hivyo kuweza kuzitofautisha simu hizo

kutokana na aina zake. Uwezo wa kutambua maumbo ya simu ungewawezesha kutambua picha iliyokuwa imetolewa kwenye swali na kuweza kuiainisha. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 91,365, sawa na asilimia 52.3 waliweza kutambua kwa usahihi kuwa picha hiyo ilikuwa ni ya “simu ya mezani”. Inawezekana utambuzi huo ulisababishwa na wanafunzi kuelewa aina za simu kwa kusoma darasani lakini pia kwa kuziona wakati wa matumizi yake nyumbani na mazingira mengine kama vile ofisini na shuleni. Kwa upande mwingine, wanafunzi 75,876, sawa na asilimia 43.4, walishindwa kuainisha picha hiyo kwa usahihi, jambo linaloashiria kuwa hawakuwa na maarifa na ujuzi wa aina za simu. Wanafunzi wengine 7,618, sawa na asilimia 4.4, hawakujibu swali hilo. Kielelezo Na. 8 kinaonesha mchanganuo wa majibu ya wanafunzi.




***Kielelezo Na 8:*** Ufaulu wa wastani wa asilimia 52.3 ya wanafunzi.

**Swali la 25:** Faida mojawapo ya kompyuta ni __________

Swali hili lilikuwa linahitaji wanafunzi wawe na maarifa ya kutosha kuhusu faida za matumizi ya kompyuta. Kati ya faida nyingi za kutumia kompyuta, wanafunzi walitakiwa kutoa faida moja tu.

Pamoja na kwamba swali hilo lilikuwa na wigo mpana wa majibu bado ufaulu wake haukuwa wa kuridhisha. Wanafunzi 36,713, sawa na asilimia 21.0, ndio walioweza kutoa faida za kompyuta kwa usahihi. Kwa upande mwingine, wanafunzi 130,438, sawa na asilimia 74.6, walishindwa kutoa faida za matumizi ya kompyuta. Kiwango hicho kikubwa cha wanafunzi walioshindwa kutoa faida za matumizi ya kompyuta kinaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya kompyuta na matumizi yake. Aidha, Wanafunzi 7,608, sawa na asilimia 4.4, hawakujibu swali hilo. Kielelezo Na. 9 kinaonesha mchanganuo wa majibu ya wanafunzi katika swali hili.




***Kielelezo Na 9:*** Ufaulu hafifu wa asilimia 21.0 tu ya wanafunzi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KATIKA KILA MADA ILIYOPIMWA

Jumla ya mada 8 zilipimwa katika upimaji wa somo la TEHAMA. Kwa ujumla, katika somo la TEHAMA ufaulu katika mada ulikuwa katika makundi mawili; mada ambazo ufaulu ulikuwa mzuri na mada

ambazo ufaulu ulikuwa wa wastani. Hapakuwa na mada ambazo ufaulu wake ulikuwa hafifu. Kati ya mada nane zilizopimwa, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa wa kiwango kizuri katika mada tano. Mada hizo ni pamoja na Mawasiliano kwa Njia za Alama, Matumizi ya Maktaba, Njia za Mawasiliano, Matumizi ya Vyombo vya Habari, na Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano.

Mada ya Mawasiliano kwa Njia ya Alama ilikuwa na swali moja. Wanafunzi katika swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri cha Asilimia 85.1. Ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri pia katika mada ya Matumizi ya Maktaba ambayo ilikuwa na maswali mawili asilimia 72.5 ya wanafunzi walifaulu vizuri. Mada hii ilikuwa ya maswali mawili. Aidha, wanafunzi walifanya vizuri pia katika mada ya Njia za mawasiliano ambapo wanafunzi asilimia 72.8 walifanya vizuri. . Mada nyingine ambayo wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri ni mada ya Matumizi ya Vyombo vya Habari ambayo wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri cha asilimia 69.8. Wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri pia cha asilimia 59.8, katika mada ya Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano.

Katika mada tatu za Kompyuta na Matumizi Yake, Simu na mada ya Mawasiliano kwa Njia ya Maandiko, wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani. Mada ya Kompyuta na Matumizi Yake ilikuwa na jumla ya maswali 8, ambapo wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha asilimia 40.8. Kwa upande mwingine, wanafunzi pia walifaulu kwa kiwango cha wastani ambapo asilimia 37.3 ya wanafunzi walifaulu katika mada ya Simu ambayo ilikuwa na maswali matano. Mada ambayo ilionekana kuwa changamoto kwa wanafunzi ni ile ya Mawasiliano kwa Njia ya Maandiko ambayo ingawa walifaulu kwa kiwango cha wastani (29.9%), ufaulu wake ulikuwa wa chini kuliko

mada zingine zote. Kiambatisho A kinaonesha ufaulu wa kila mada kwa muhtasari. Mada ambazo wanafunzi wamefaulu kwa kiwango kizuri zimetiwa kivuli kwa rangi ya kijani, na mada ambazo wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani zimetiwa kivuli kwa rangi ya njano.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa maswali ya upimaji katika somo la TEHAMA unaonyesha kuwa maswali 9 kati ya 25 katika somo hili la TEHAMA yalijibiwa vizuri. Maswali 16 yaliyobaki ya mada ya ‘Kompyuta na Matumizi Yake, Simu na mada ya mawasiliano kwa njia ya maandiko yalijibiwa kwa kiwango cha wastani. Mada zilizojibiwa vizuri ni pamoja na, Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano, Matumizi ya Vyombo vya Habari, Njia za Mawasiliano, Matumizi ya Maktaba na Mawasiliano kwa Njia ya Alama. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na uboreshaji wa miundombinu ya shule ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA. Aidha, ni matumaini ya Baraza kuwa mada zilizoonekana kuwa na changamoto katika ufaulu wake zitaangaliwa ili kubaini sababu za ufaulu huo wa wastani.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu na ufaulu kwa ujumla katika somo la TEHAMA Baraza la Mitihani linashauri yafuatayo:

(a) Walimu waweke mkazo katika kufundisha mada ambazo ufaulu wa wanafunzi katika mada hizo, katika upimaji wa mwaka 2015, ulikuwa wa wastani, hasa mada ya mawasiliano kwa Njia ya Maandiko, Simu, na mada ya Kompyuta na Matumizi yake.

(b) Wanafunzi waelimishwe namna ya kusoma maswali kwa umakini ili waweze kubaini matakwa ya kila swali na hivyo kuwawezesha kuyajibu kwa ufasaha badala ya kuharakisha na kisha kutoa majibu yasiyo sahihi.

(c) Wanafunzi wahimizwe kusoma vitabu vya kiada na ziada ili waweze kujiongezea maarifa yatakayowawezesha kujibu maswali vizuri wakati wa upimaji.

(d) Mamlaka zinazohusika zifuatilie ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi katika somo la TEHAMA ili kuweza kubaini changamoto mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi, na hatimaye kuboresha mazingira ya ufundishaji, na ujifunzaji hivyo kuongeza kiwango cha ufaulu.

Kiambatisho A

**UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA MADA KATIKA SFNA 2015, SOMO LA TEHAMA**

| Na | MADA | UPIMAJI WA SFNA 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya ufaulu | | |
| 1. | Mawasiliano kwa Njia ya Alama | 17 | 85.1 | 85.1 | Mzuri |
| 2. | Matumizi ya Maktaba | 6 | 90.6 | 77.5 | Mzuri |
| | | 18 | 64.6 | | |
| 3. | Njia za Mawasiliano | 3 | 89.7 | 72.8 | Mzuri |
| | | 9 | 72.8 | | |
| | | 16 | 75.2 | | |
| | | 19 | 53.7 | | |
| 4. | Matumizi ya Vyombo vya Habari | 7 | 69.8 | 69.8 | Mzuri |
| 5. | Matumizi ya Vituo vya Habari na Mawasiliano | 5 | 59.8 | 59.8 | Mzuri |
| 6. | Kompyuta na Matumizi yake | 20 | 64.0 | 40.8 | Wastani |
| | | 10 | 45.0 | | |
| | | 11 | 27.2 | | |
| | | 12 | 34.5 | | |
| | | 13 | 34.0 | | |
| | | 14 | 22.9 | | |
| | | 15 | 69.2 | | |
| | | 25 | 21.0 | | |
| 7. | Simu | 1 | 35.6 | 37.3 | Wastani |
| | | 2 | 43.7 | | |
| | | 8 | 63.8 | | |
| | | 21 | 22.2 | | |
| | | 24 | 21.0 | | |
| 8. | Mawasiliano kwa njia ya Maandiko | 4 | 51.6 | 29.9 | Wastani |
| | | 22 | 36.2 | | |
| | | 23 | 1.6 | | |

**Kiambatisho B**

**KIELELEZO KINACHOONESHA ASILIMIA YA WANAFUNZI WALIOFAULU KATIKA KILA MADA**




***Kiambatisho B:*** ***u***faulu katika mada tatu ni wa wastani. Kwa upande mwingine, ufaulu katika mada tano ni mzuri.